# ARDHI NI UHAI

HAKIARDHI ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 13 JANUARI - APRILI 2015


# KULIKONI MIGOGORO YA WAKULIMA NA WAFUGAJI HAIISHI?

*Na: Cathbert Tomitho*



*Baadhi ya wananchi wa Dumila Morogoro katika moja ya tukio la mgogoro wa Ardhi kati ya wakulima na wafugaji*

Migogoro baina ya makundi ya watumiaji wa ardhi nchini Tanzania imekuwa ikichukua sura tofauti-tofauti kila wakati kuanzia kwenye vyanzo vya migogoro husika, utatuzi wake na athari zinazoambatana na migogoro husika. Kwa upande wa wakulima na wafugaji, migogoro hii imekithiri na hata kufikia hatua ya watu kuamini kuwa haiwezi kupata susluhu ya kudumu. Makala hii inachambua kwa undani vyanzo kadhaa vya migogoro hii na kupendekeza hatua muhimu za kuchukua ili kuitokomeza kabisa.

Mojawapo ya vyanzo hivyo ni mapungufu ya kimaudhui katika sera na sheria zinazohusiana na usimamizi na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Kimsingi, mapungufu haya ya kisheria yanatokana na kukosekana kwa ushiriki mkamilifu wa wananchi katika michakato ya utungaji wa sheria wakati sheria zinazotungwa zikigusa maisha yao ya kila siku. Kutopewa fursa ya kutoa maoni pamoja na kutozingatiwa kwa maoni wanayoyatoa kumechangia wahusika kujiona wao hawathaminiwi na wakati mwingine kujichukulia hatua mkononi kama njia ya kulazimisha kutambulika kwao. Kwa mfano, katika sera na sheria za ardhi, hakuna kipengele kinachohusu kutambua, kulinda na kusimamia mfumo wa ufugaji wa asili wakati ndio mfumo unaotumiwa na wafugaji walio wengi nchini.

Changamoto nyingine katika eneo la sheria ni utekelezaji hafifu wa sheria zilizokwishatungwa.

*Inaendelea uk. 3 >>*

YALIYOMO


- KULIKONI MIGOGORO YA WAKULIMA NA WAFUGAJI HAIISHI? 1
- TUME NA KAMATI TEULE ZINA NAFASI GANI KATIKA UTATUZI WA MIGOGORO YA WAKULIMA NA WAFUGAJI? 1 - 4
- NAFASI YA MABARAZA YA ARDHI 5
- ATHARI ZA MIGOGORO YA ARDHI 6
- MAONI YA MWANANCHI 7
- OPERESHENI ONDOA WAFUGAJI 8
- KONA YA SHERIA 10


# TUME NA KAMATI TEULE ZINA NAFASI GANI KATIKA UTATUZI WA MIGOGORO YA WAKULIMA NA WAFUGAJI?


*Na: Yefred Myenzi*

Serikali imekuwa na jitihada nyingi katika kukabiliana na migogoro ya ardhi kati ya makundi mbalimbali nchini. Moja ya jitihada hizo ni kuundwa kwa tume na kamati teule za uchunguzi wa masuala husika na kuyatolea mapendekezo kwa ajili ya utekelezaji. Tume na kamati hizi zimekuwa zikiundwa ama na Bunge au Serikali. Hata hivyo, kumekuwa na hoja nyingi kuhusu umadhubuti wa tume na kamati teule hizo kutokana na ukweli kuwa, mengi ya mapendekezo yake, yamekuwa hayafanyiwi kazi ili kukabiliana na migogoro ya ardhi inayozidi kukithiri nchini. Makala hii inaonyesha baadhi tu ya kamati teule na tume zilizowahi kuundwa lakini mapendekezo yake yakabaki katika makabati ya walioziunda bila kusaidia tatizo la msingi la kuundwa kwake.

Mnamo mwaka 1991 serikali iliunda tume ya Rais ya uchunguzi juu ya masuala ya ardhi iliyokuwa chini ya Profesa Issa Shivji baada ya kubaini kukithiri kwa migogoro ya ardhi. Tume hii ilizunguka nchi nzima kuhojiana na wananchi na kutoa mapendekezo ya

> *"Makala hii inaonyesha baadhi tu ya kamati teule na tume zilizowahi kuundwa lakini mapendekezo yake yakabaki katika makabati ya walioziunda bila kusaidia tatizo la msingi la kuundwa kwake.*

*Inaendelea uk. 4 >>*




**ARDHI NI UHAI** Ni jarida la Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI) ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka.

Kusudi kubwa ni kuwapa wadau wa Taasisi hii taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ardhi

**MHARIRI**
Yefred Myenzi


**BODI YA WAHARIRI**
Yefred Myenzi - M/Kiti
Cathbert Tomitho - Mjumbe
Nakamo Tenende - Mjumbe
Grace Mpangala - Mjumbe
Mchapishaji - HAKIARDHI
Mchapaji - iPrint
Msanifu - Bakari Kacheuka

**UJUMBE WA BODI KWA WASOMAJI**
WASOMAJI wa jarida hili mnakaribishwa kutoa michango yenu kwa kuuliza maswali, kutoa ushauri, maoni, au kwa kuandika makala (zisizozidi kurasa tatu) kwa mhariri kupitia anuani zifuatazo:

HAKIARDHI
Land Rights Research & Resources Institute

Kitalu No.236 Block 47 Sinza Mori, Mkabala na Wanyama Hotel, S.L.P 75885, Dar es Salaam
Simu +255 22 2771360/ 0784 646752,
Nukushi: +255 22 2771362
Baruapepe: info@hakiardhi.org,
Tovuti: www.hakiardhi.org

TAHARIRI



# SERIKALI IONYESHE DHAMIRA YA KWELI YA KUTOKOMEZA MIGOGORO YA ARDHI NCHINI.

*Migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji ina historia ndefu Tanzania.*

Migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji ina historia ndefu Tanzania. Hivi Karibuni, Bunge la Jamhuri liliunda kamati teule iliyochunguza migogoro kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi na kubainisha kuwa, migogoro ya ardhi inayoendelea leo, imekuwepo kwa muda mrefu ikiwemo ile iliyoanza tangu mwaka 1966. Katika toleo hili la jarida letu, tumejadili mambo mengi kuhusiana na vyanzo vya migogoro ya ardhi na athari zake lakini tukijikita zaidi katika kuitazama dhamira ya serikali ya kutokomeza migogoro hii. Wachambuzi wa makala za toleo hili wamejaribu kuonyesha jitihada za serikali na Bunge katika kutunga sera na sheria za ardhi za mwaka 1995 na 1999, kuweka mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa sheria ya mwaka 2002 na hata kuunda tume na kamati mbalimbali kushughulikia migogoro ya ardhi pale ilipojitokeza.

Hata hivyo, uchambuzi unaonyesha kuwa, serikali imekosa nia ya dhati ya kuhakikisha migogoro ya ardhi inakwisha kutokana na ukweli kuwa, imeshindwa kupanga matumizi ya ardhi kwa kuzingatia misingi ya usawa na haki kati ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine tangu sheria mpya zilipotungwa. Matokeo yake, wazalishaji hawa wa msingi, wamekosa uhakika wa milki ya ardhi kwa kuwa wakati wowote matumizi yanaweza kubadilika wakamilikishwa watumiaji wengine hasa wawekezaji na wenye nguvu za kiuchumi katika jamii.

Taarifa ya kamati teule ya Bunge iliyotolewa hivi karibuni, inaonyesha orodha ya majina ya wamiliki wa mashamba makubwa yasiyoendelezwa wengi wakiwa wanasiasa, wafanya biashara wakubwa na taasisi za serikali. Uhodhi huo wa ardhi unafanywa huku sheria zikieleza bayana kuwa walipaswa kuwa wamenyang'anywa baada ya miezi 36 kwa kukiuka sharti la kutoendeleza ardhi wanayomiliki. Haielekweki ni kwanini serikali inapata ugumu wa kutekeleza sheria hiyo.

Kumekuwa pia na shutuma za kushindwa kutoa huduma au kusikiliza kero kwa wakati hadi mambo yanapoharibika. Kwa mfano, mwaka 2000 yalitokea mauaji kwa wakulima 36 wa Kijiji cha Rudewa Mbuyuni Wilaya ya Kilosa yaliyofanywa na wafugaji. Katika kufuatilia tukio hili, ilibainika kuwa taarifa za mgogoro huo zilikuwepo katika ngazi mbalimbali za uongozi wa Wilaya hiyo kwa zaidi ya miaka mitano na hakuna hata ofisi moja iliyotimiza wajibu wake hadi mauaji yakatokea. Mwaka 2013, mauaji kama hayo yakatokea katika bonde la Mgongola Wilaya ya Mvomero huku serikali ya Wilaya ikiwa na taarifa za kufukuta kwa mgogoro huo kwa muda bila kuchukua hatua.

> UCHAMBUZI UNAONYESHA KUWA, SERIKALI IMEKOSA NIA YA DHATI KATIKA KUHAKIKISHA MIGOGORO YA ARDHI INAKWISHA

Ndiyo maana tunao ujasiri wa kutamka kuwa serikali imekosa dhamira na utashi wa kumaliza migogoro ya ardhi kwa kushindwa kuitikia kwenye taarifa za migogoro kwa wakati, kutoa huduma stahiki kwa usawa kati ya watumiaji mbalimbali wa ardhi, kusimamia utekelezaji wa sheria kikamilifu na kulinda maisha na mali za wananchi wake kama ilivyoainishwa kwenye katiba ya nchi. Mtizamo hasi dhidi ya wafugaji na mfumo mzima wa ufugaji wa asili nchini usipobadilika, tutaendelea kushuhudia migogoro ya ardhi isiyo na mwisho. Ufike wakati sasa serikali ionyeshe dhamira ya dhati ya kumaliza migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji kwa kuchukua hatua stahiki na kwa wakati.

**Yefred Myenzi**
**MHARIRI**

» Inatoka uk. 1

# KULIKONI MIGOGORO YA WAKULIMA NA WAFUGAJI HAIISHI?

Sheria ya Ardhi namba 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 zote za mwaka 1999, Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi namba 6 ya mwaka 2007 pamoja na Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi namba 2 ya mwaka 2002 zimekuwa na vipengele vinavyokiukwa au kutotekelezwa kabisa. Kwa mfano, kutokutekelezwa ipasavyo kwa mpango wa matumizi ya ardhi kwenye vijiji vingi nchini kumekuwa kukichochea migogoro ya wakulima na wafugaji. Tafiti zinaonyesha kuwa utekelezwaji madhubuti wa mpango wa matumizi ya ardhi ungesaidia kupunguza migogoro baina ya makundi haya kutokana na kila kundi kutengewa ardhi kwa ajili ya matumizi yake pasipo muingiliano.

Vilevile mgawanyo usio sawa wa rasilimali ardhi baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi umekuwa kichocheo kingine cha migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Kukua kwa soko huria katika uchumi wa dunia kumeleta wimbi kubwa la uwekezaji katika ardhi na rasilimali nyingine. Pale wawekezaji wanapoonekana kupewa kipaumbele zaidi ya wenyeji inakuwa kichocheo kwa makundi mengine ya watumiaji wa ardhi hasa wakulima na wafugaji kujiona wanabaguliwa au kuona wanakosa maeneo ya kutosha ya kuendesha shughuli zao hasa kilimo na ufugaji. Mfano katika wilaya za Ngorongoro, Mbarali, Mvomero, Kilosa, Morogoro Vijijini, Kilombero, Ulanga, Bagamoyo na Mkuranga kumekuwa na wimbi kubwa la wawekezaji na ugawaji mkubwa wa ardhi usiozingatia maslahi ya wakulima na wafugaji wa maeneo hayo.

> MARA NYINGINE KATIKA MKUTANO MKUU WA KIJIJI AKIDI HAIFIKIWI LAKINI VIONGOZI HAWA HUORODHESHA MAJINA NA IDADI YA UONGO KWA KUCHUKUA MAHUDHURIO YA MIKUTANO MINGINE ISIYOHUSIANA NA UGAWAJI ARDHI KWA MWEKEZAJI.

Kukosekana kwa utashi wa kisiasa ni kichocheo kingine cha migogoro baina ya wakulima na wafugaji nchini. Kumekuwa na kauli pamoja na matendo yanayochochea migogoro kutoka miongoni mwa wanasiasa kama madiwani, wabunge, wakuu wa wilaya na wakuu wa mikoa. Baadhi ya viongozi hawa wamekuwa wakitumia kauli za kisiasa katika maamuzi yanayohusiana na usimamizi na utatuzi wa migogoro ya ardhi ambayo matokeo yake ni kuchochea migogoro zaidi baina ya watumiaji wa ardhi. Kwa mfano gazeti la Majira la Januari 1, 2011 liliripoti kuhusiana na madiwani wa wilaya ya Hanang ambao walilalamikiwa na kundi la wafugaji kwa kile kilichoonekana kuwapendelea wakulima katika maamuzi ya matumizi ya ardhi hususan mgawo wa mashamba ambayo serikali iliyarejesha kwa wananchi baada ya NAFCO kufilisika.

Halikadhalika maamuzi yasiyo na utafiti wa kina ya viongozi na taasisi za serikali yanayolenga katika usimamizi na uhifadhi wa mazingira yamekuwa yakichochea migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Kwa mfano kumekuwa na maamuzi ya mara kwa mara ya operesheni za kuhamisha wafugaji na wakulima kutoka kwenye maeneo ambayo wamekuwa wakiyatumia kwa kilimo na ufugaji. Mwaka 2006, serikali ilifanya operesheni ya kuwahamisha wafugaji katika eneo la Bonde la ardhi Oevu la Ihefu wilayani Mbarali kwa lengo la kuhifadhi mazingira. Operesheni hii ilisababisha wafugaji na mifugo yao kusambaa maeneo mbalimbali nchini pasipo utaratibu maalum na kusababisha migogoro baina ya wakulima na wafugaji kwenye maeneo mengine. Kwa mfano migogoro ya makundi haya katika wilaya za Mkuranga, Kilwa, Bagamoyo, Ulanga, Kilombero na maeneo mengine nchini kuanzia mwaka 2007 hadi sasa, imekuwa ikihusishwa moja kwa moja na athari za operesheni hii.

Sababu nyingine ni mitazamo mibaya juu ya baadhi ya mifumo ya uzalishaji mali kama vile ufugaji na ukulima. Kwa mfano kumekuwa na dhana iliyojengeka miongoni mwa wakulima kuwa wafugaji wanaofanya ufugaji wa asili wanafanya shughuli ambayo haina tija wala maslahi kwa jamii zaidi ya uharibifu wa mazingira. Vilevile kumekuwa na mtazamo mbaya miongoni mwa wafugaji kuwa kilimo ni kazi isiyokuwa na tija wala maslahi ya kutosheleza kama ulivyo ufugaji kwa maana hiyo ufugaji ni bora kuliko kilimo. Mitizamo hii kwa njia moja au nyingine huchochea chuki na uhasama baina ya makundi husika na hivyo kurahisha kuibuka kwa migogoro ya mara kwa mara.

Mabadiliko ya tabianchi ni chanzo kingine cha migogoro hii kutokana na ukweli kuwa uharibifu wa mazingira umekuwa na madhara ya moja kwa moja kwenye matumizi ya ardhi. Mojawapo ya athari za mabadiliko ya tabianchi ni pamoja kuongezeka kwa ukame na hivyo kupunguza matumizi ya asili ya ardhi. Katika maeneo ambayo yamekumbwa na mabadiliko ya tabianchi waathirika wakubwa wamekuwa ni wakulima na wafugaji hasa ikizingatiwa kuwa watumiaji hawa hutegemea mvua za asili kwa mazao yao na kupata malisho ya mifugo. Mabadiliko ya tabianchi yamepunguza kwa kiasi kikubwa nyanda za malisho hivyo kulazimisha wafugaji kuhamisha mifugo yao kutoka eneo moja hadi jingine. Vilevile wakulima wamekuwa wakipanua mashamba yao hadi katika hifadhi ya maeneo ya ufugaji ili kupata ardhi yenye rutuba.

Kwa ujumla, utatuzi wa migogoro ya ardhi baina ya makundi ya wakulima na wafugaji unategemea ustadi wa serikali na wadau wengine katika sekta ya ardhi na mazingira katika kupambana na vyanzo mbalimbali vya migogoro hii. Utashi wa serikali ni muhimu katika utatuzi wa migogoro kutokana na nafasi yake katika kutunga na kutekeleza sera na sheria za ardhi na rasilimali nyinginezo kama misitu, gesi, madini na maji. Hata hivyo, dhamira ya wananchi hususan wakulima na wafugaji kutokomeza migogoro ni jambo la msingi kwa kuwa wao ndio huathirika na matokeo ya migogoro kuliko hata serikali. Hivyo, wakulima na wafugaji hawana budi kubadili mitizamo yao juu ya migogoro ya ardhi na kuchukua hatua ya kusema migogoro sasa basi kwa vitendo.

» Inatoka uk. 1

namna ya kuunda mfumo mpya wa milki ya ardhi ikiwemo kuandaa sera na sheria mpya za ardhi pamoja na kuweka mfumo mbadala wa utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Licha ya baadhi ya mapendekezo ya tume hii kuzingatiwa, lakini migogoro ya ardhi imeendelea kuongezeka kila mwaka. Tathmini nyingi zimeonyesha kuwa, mapendekezo ya msingi ya kugatua mamlaka ya utawala wa ardhi na kuweka katika vyombo vyenye ushiriki na uwakilishi mpana wa wananchi hayakuzingatiwa. Mamlaka ya utawala wa ardhi hasa umilikishaji, utwaaji, uhamishaji wa milki na hata ufutaji wa hati yanapokuwa mbali na wananchi, uwezekano wa kutokea migogoro ni mkubwa, na ndivyo ilivyo kiuhalisia.

Tume nyingine iliyokuwa nchini ya jaji Othmani Chande (sasa ni jaji Mkuu), iliundwa mwaka 2006, ili kushughulikia malalamiko ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu kwa wafugaji waliokuwa wakihamishwa kutoka bonde la Ihefu wilayani Mbarali mkoa wa Mbeya kwenda mikoa ya Lindi na Mtwara. Tume iliundwa kutokana na baadhi ya taarifa za kitafiti na za ufuatiliaji wa operesheni hiyo kubainisha kuwa wafugaji walipata madhara makubwa yaliyotokana na matumizi makubwa ya nguvu za jeshi la polisi, yakiwemo, kufa kwa mifugo kutokana na safari ndefu kutoka Ihefu hadi mikoa ya kusini, faini kubwa walizokuwa wakitozwa na kusambaratika kwa familia baada ya kutawanywa na jeshi la polisi.

Licha ya tume hiyo kutoa ripoti na kuikabidhi kwa Rais tangu mwaka huo wa 2006, haijawahi kutolewa hadharani wala mapendekezo yake kufanyiwa kazi pamoja na wabunge kutoka jamii za kifugaji kuifuatilia mara kwa mara. Ni dhahiri kwamba, kuenea kwa migogoro maeneo ya kusini na baadhi ya wilaya za mkoa wa Morogoro na Pwani hakuwezi kutenganishwa na athari za operesheni hiyo, maana wafugaji waliotoka Ihefu walielekea maeneo hayo.

> **NI JUKUMU LETU SOTE KUHAKIKISHA KUWA WANYAMAPORI NA MAPORI YAO YANALINDWA KWAAJILI YA VIZAZI VYA SASA NA VIJAVYO.**

## TUME NA KAMATI TEULE ZINA NAFASI GANI KATIKA UTATUZI WA MIGOGORO YA WAKULIMA NA WAFUGAJI?



*Wananchi wa kijiji cha Kidabaga katika moja ya mikutano na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo - Iringa*

Mwaka 2009 matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu kwa wafugaji hasa waishio Loliondo wilaya ya Ngorongoro yalikithiri baada ya kuchomwa kwa maboma takribani 200 ya wafugaji wa vijiji vinavyozunguka kitalu cha OBC na kuathiri maisha ya zaidi ya wananchi 10,000 wanaoishi vijiji hivyo. Kamati ya Bunge ya ardhi, maliasili na mazingira ilitembelea maeneo hayo, kuzungumza na wananchi na hatimaye kuandaa taarifa iliyosubiriwa kwa hamu kuwasilishwa bungeni. Hata hivyo, taarifa hiyo haijawahi kuwekwa hadharani bila sababu za msingi. Katika hali ya kawaida, wananchi wanabaki na maswali vichwani kuhusiana na serikali na wakati mwingine Bunge kutumia fedha na rasilimali za umma bila kutoa matokeo ya uchunguzi unaokuwa umesubiriwa kwa hamu kulingana na matukio husika.

Kwa miaka ya hivi karibuni kuanzia 2011 hadi 2015 kumekuwa na mfululizo wa migogoro ya ardhi na mapigano kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi katika maeneo ya Rufiji, Kiteto, Mvomero na Kilosa ambayo yamesababisha vifo kwa watu wasio na hatia na upotevu wa mali zao.

Mfululizo wa matukio hayo ulilisukuma Bunge kuunda kamati teule ya kuchuguza migogoro hiyo tarehe 9 Novemba 2013 ambayo hatimaye iliwasilisha taarifa yake rasmi tarehe 6 Februari 2015 bungeni ikiwa imesheheni sababu, ufafanuzi, vielelezo na mapendekezo yanayoweza kusaidia kutokomeza migogoro ya ardhi nchini. Taarifa inaonyesha jinsi serikali na taasisi zake zilivyoshindwa kutimiza wajibu wake hadi kusababisha migogoro yenye athari kubwa kwa wananchi kutokea.

Tofauti na matarajio kuwa bunge lingeweka mikakati ya kuibana serikali kutimiza yale ambayo taarifa inaonyesha wameshindwa kutimiza, serikali ikaamua kujibebesha jukumu la kuyafanyia kazi na hatimaye kupunguza makali ya kazi yote ya kamati teule ya Bunge. Suala la kujiuliza ni je, baada ya kuona mwenendo wa kamati teule na tume za serikali na za bunge, tutarajie nini cha tofauti katika taarifa ya kamati hii kutoka kwa serikali?

Baada ya kusoma mambo yaliyoainishwa na kamati na kushuhudia uhusika wa serikali na taasisi zake katika migogoro mingi ama kwa kutotimiza wajibu au kwa kupuuzia mambo kwa makusudi, siamini wala sioni tija ya kuunda tume na kamati teule za bunge kwa matarajio kuwa zitasaidia kumaliza matatizo yanayoikabili jamii ikiwemo migogoro sugu ya ardhi iliyopoteza maisha na mali za wananchi wa Tanzania. Badala yake, fedha zinazotumika kwa tume na kamati teule hizo, zielekezwe katika kuimarisha mifumo ya usismamizi wa ardhi na kutoa huduma kwa wazalishaji wa msingi wakiwemo wakulima na wafugaji.

# UTATUZI WA MIGOGORO YA WAKULIMA NA WAFUGAJI: Mabaraza na Mahakama za Ardhi vina nafasi gani?

*Na. Beatha Fabian*

Wakulima na wafugaji nchini Tanzania wamekuwa na historia ndefu ya migogoro na mapigano ambayo yamekuwa yakisababisha mauaji ya watu wengi. Migogoro hii ambayo kiini chake ni ardhi na rasilimali kama malisho na maji, imekuwa ikiongezeka siku hadi siku katika maeneo mbalimbali. Baadhi ya maeneo ambayo yamekithiri kwa migogoro kwa takribani miongo mitatu iliyopita ni pamoja na; Monduli, Loliondo, Arumeru, Babati, Kiteto na Hanang kwa Mikoa ya Arusha na Manyara, Kilosa, Mvomero na Morogoro Vijijini kwa Mkoa wa Morogoro na maeneo ya Mbarali, Pawaga, Mpanda na Chunya kwa Mikoa ya Iringa, Mbeya na Katavi. Lakini kwa siku za karibuni, migogoro imezidi kusambaa hadi Wilaya za Kilombero na Ulanga na hatimaye mkoa wa Pwani hasa Wilaya za Kisarawe, Rufiji na Bagamoyo ambako zamani haijawahi kuwepo kabisa.

Kwa muda mrefu tangu mapema miaka ya 90, kumekuwa na jitihada nyingi za serikali na asasi za kiraia kutatua migogoro hii, lakini hata hivyo hazijaweza kuzaa matunda kwa kuwa migogoro hii imeendelea kusababisha madhara makubwa yakiwemo mauaji, upotevu wa mali, muda na hata nguvu kazi na kuongeza uhasama katika jamii. Jitihada za serikali zinaonekana katika sheria za ardhi za mwaka 1999 ambazo zimeweka utaratibu wa kutatua migogoro inayohusu mipaka ya vijiji kiutawala kuanzia ngazi ya kijiji hadi kwa waziri mwenye dhamana ya ardhi. Lakini hata hivyo, kumekuwa na migogoro ya mipaka ya vijiji ambayo imedumu kwa zaidi ya miaka 30 bila kutatuliwa licha ya jitihada zilizofanyika kujaribu kumaliza migogoro hiyo.

Hali hiyo ndiyo iliisukuma serikali kuandaa sheria ya mahakama na mabaraza ya ardhi namba 2 ya mwaka 2002 ambayo ilipitishwa na Bunge na kuanza kutumika rasmi mwezi Oktoba 2003. Sheria hii inaunda mabaraza kuanzia ngazi ya kijiji hadi Wilaya na kuhusisha mhimili wa mahakama baada ya ngazi hiyo. Mabaraza hayo ni pamoja na Baraza la Ardhi la Kijiji, Baraza la Kata na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya. Baada ya Baraza hili, muundo wa mabaraza hujumuishwa kwenye muundo wa Mahakama kuanzia Mahakama Kuu na hatimaye Mahakama ya Rufani.

Nia ya kuanzisha mabaraza haya ni kuhakikisha kuwa utatuzi wa migogoro unakuwa wa haraka na wa haki. Sababu nyingine ni kuongeza ushiriki wa wananchi katika utatuzi wa migogoro na kupunguza mrundikano wa kesi katika mahakama za kawaida pamoja na gharama za uendeshaji wa kesi hizo. Ndio maana Mabaraza ya ardhi ya vijiji na yale ya Kata hutumia taratibu za kimila katika usuluhishi wake. Mabaraza haya yanaundwa na wajumbe ambao ni wanajamii wanaochaguliwa na kuafikiwa na jamii nzima kidemokrasia. Baraza la ardhi la Kijiji lina wajumbe 7 kati yao wanawake wasipungue 3. Kwa upande wake, Baraza la kata linaundwa na wajumbe kati ya 5 hadi 8 na kati yake wanawake wasipungue 3.

Kwa kuwa wajumbe wa mabaraza ni wanajamii wenyewe, wanaotumia taratibu za kimila kufikia suluhu, mara nyingi inashauriwa kupata wajumbe mchanganyiko wakiwemo watu wa makamo wanaoheshimika na wanaozielewa na kusimamia sheria za kimila pamoja na vijana ili kuhakikisha mwendelezo wa hekima za usuluhishi unakuwepo. Kwa ujumla, mafanikio ya mfumo huu wa sheria katika kudhibiti migogoro hii ambayo ni ya kirasilimali utategemea uhiari wa wakulima na wafugaji pamoja na uwezo wa utekelezaji wa haya mabaraza ambayo kazi kuu ni kupatanisha na kusuluhisha.

Tofauti na ngazi za juu za mahakama ambapo wahusika tu ndio wanaoruhusiwa kushiriki katika shauri, ngazi hii ya usuluhishi inaruhusu pia watu walio nje ya mgogoro na waliokubaliwa na pande zote mbili kuwezesha majadiliano na kufikia uamuzi kati ya walalamikaji. Kwa upande wa mijini, halmashauri za miji, majiji, na manispaa, hutumia Mabaraza ya Kata kwani nayo hupokea migogoro ya mashamba, mimea na hata malisho ya mifugo. Mabaraza haya pia hutumia taratibu za kimila kama mwongozo katika upatanishi au kufikia suluhisho baina ya walalamikaji.

Kwa upande wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, mahakama kuu na mahakama ya Rufani, taratibu za kisheria ndizo hutumika ziadi. Ngazi hizi zinajikita zaidi katika vifungu vya sheria kubaini makosa ya kiuandishi, maudhui ya mawasilisho ya kesi na ushindi katika hoja za utetezi tofauti na dhamira ya kuhakikisha kuwa suluhu inapatikana inayoongoza mabaraza katika ngazi za kijiji na Kata.

Hivyo basi, mabaraza na mahakama za Ardhi yana nafasi ya kipekee sana katika kusuluhisha migogoro baina ya wakulima na wafugaji isipokuwa ipo haja ya kutazama upya muundo wake na taratibu za utatuzi wa migogoro kwani ni dhahiri kwamba, kumekuwa na ongezeko la mapigano kati ya wafugaji na wakulima wakigombea ardhi ya kilimo na ya malisho ya mifugo, na utatuzi wa migogoro hii kwa kufuata mila pekee yake unaonekana haujitoshelezi. Mapendekezo mengine ya kuboresha mfumo huu ni pamoja na:

Kwanza, wajumbe wa mabaraza wanapaswa wapewe elimu zaidi ili kupanua wigo wa ujuzi wao kuhakikisha jitihada za mapatano na usuluhishi zinamaliza migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Pili, mabaraza yatengewe pesa ya kutosha katika bajeti za Halmashauri za Wilaya husika ili yaweze kujiendesha badala ya kutegemea walalamikaji katika shauri kugharimia usikilizaji shauri. Hali hii inasababisha haki isionekane kuwa inatendeka pale walalamikaji wanapokosa fedha za kufungulia mashauri.


Tatu, Mahakama na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yapunguze gharama kubwa za uandikishwaji na mwenendo wa kesi ili kupanua wigo wa utatuzi wa migogoro ya aina hii mahakamani tofauti na inavyofanyika sasa yaani kuundiwa Tume mbalimbali kuishughulikia au pengine viongozi wa siasa na serikali kuhusika katika utatuzi wa migogoro hii.

Nne, ni muhimu kwa jamii kujenga utamaduni wa kuheshimu na kuzingatia suluhu pamoja na hukumu zinazotolewa na vyombo hivi ili kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji. Haitakuwa na maana suluhu kufikiwa bila wahusika kuchukua hatua stahiki ikiwemo kuwajibika na kuachia maeneo pale ambapo suluhu inakuwa imefikiwa hivyo.

# ATHARI ZA MIGOGORO YA ARDHI YA WAKULIMA NA WAFUGAJI NCHINI

*Na; Cathbert Tomitho*

Kadri migogoro baina ya wakulima na wafugaji inavyoongezeka nchini ndivyo athari zinazosababishwa na migogoro hiyo zinavyokuwa nyingi. Kumekuwa na taarifa kutoka maeneo mbalimbali nchini kupitia vyombo vya habari na tafiti mbalimbali zikionyesha jinsi wananchi wanavyoathirika. Makala hii inachambua kwa undani athari za migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji.



*Kundi la wabarbaig wa wilaya ya Hanang katika mojawapo ya migogoro ya ardhi wilayani humo*

Athari ya kwanza kabisa ni upotevu wa maisha ya binadamu unaotokana na mapigano ya makundi haya. Kwa mfano, watu watano (5) waliuawa kutokana na migogoro ya wakulima na wafugaji katika wilaya ya Kilombero mwaka 2012, wananchi saba (7) waliuawa na wengine 36 kujeruhiwa mwaka 2013 Wilayani Mvomero huku mauaji mengine yakitokea mfululizo kati ya mwaka 2013/14 kwenye wilaya za Kiteto na Mvomero kutokana na migogoro ya aina hii. Mauaji haya yamesababisha hasara kubwa kwa familia na jamii kwa ujumla kama inavyochambuliwa hapa chini.

Kwanza, migogoro imerudisha nyuma maendeleo kutokana na kusababisha uharibifu wa miundombinu, makazi na hata baadhi ya watu kujificha kwa kuogopa kukamatwa kutokana na tuhuma za kuhusishwa na migogoro hiyo na hivyo kuacha shughuli za uzalishaji mali. Kwa mfano, wilaya za Kiteto na Mvomero zimekuwa nyuma kimaendeleo kutokana na migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo husababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu kama vile majosho.

Migogoro ya wakulima na wafugaji imekuwa chanzo cha upotevu wa muda mwingi pamoja na fedha. Tafiti zinaonyesha kuwa migogoro ya ardhi imekuwa ikichukua muda mrefu kupata suluhisho iwe katika taratibu za kiutawala au kwenye mahakama za ardhi. Kuna mfano hai wa kesi ya wafugaji wa Kibarbaig waliokuwa wakiongozwa na Yoke Gwako wa huko Hanang dhidi ya shirika la NAFCO ambayo ilidumu tangu mwaka 1995 hadi 2006 na hatimaye wananchi wakashindwa katika ngazi ya mahakama ya rufani. Kwa muda wote huo, muda na fedha nyingi zilitumika na kurudisha nyuma maendeleo ya wananchi.

Vilevile migogoro baina ya wakulima na wafugaji imekuwa ikichochea chuki na uhasama miongoni mwa wananchi. Tafiti zinaonyesha kuwa migogoro ya wakulima na wafugaji katika maeneo kama ya Kiteto kwenye eneo la hifadhi ya Emburoi Murtangosi na maeneo ya Kilosa na Mvomero husababishwa na uhasama uliopo baina ya wakulima na wafugaji na sababu nyingine ni za mpito tu. Uhasama huu umesababishwa na historia ya mauaji na uharibifu wa mali wa kundi moja dhidi ya jingine.

Unyanyasaji wa kijinsia ni athari nyingine inayotokana na migogoro ya wakulima na wafugaji hasa kwa upande wa wanawake na watoto. Wanawake na watoto huathirika kutokana na kutoweza kuhimili mikikimikiki ya mapigano, au kutelekezwa na wanaume wanapokwenda kwenye mapigano. Vilevile wanawake na watoto huathirika na ukosefu wa makazi pamoja na chakula kutokana na wanaume kuzikimbia familia zao kwa kuhofia kukamatwa na vyombo vya dola kwa kuhusika na mapigano.

Kwa ujumla, migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji imekuwa na athari kubwa si tu kwa makundi haya mawili ila kwa taifa kwa ujumla. Hii ni kutokana na uchumi wa nchi kukosa mchango wa makundi haya kupitia ufugaji na kilimo wakati wanapokuwa kwenye migogoro. Katika nchi nyingine za Afrika kama vile Bostwana na Ethiopia, ufugaji umechangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa uchumi wa nchi hizo kutokana na kutokuwepo kwa migogoro mingi na ya mara kwa mara inayowahusisha makundi yote. Kwa Tanzania, suala hili limekuwa gumu kutokana na muda mwingi na rasilimali nyingi kutumika katika kutatua migogoro ya ardhi.

Ni jukumu la serikali pamoja na wadau wengine hasa asasi za kiraia kuhakikisha kuwa kunafanyika marekebisho ya sera na sheria pamoja na kutekeleza sheria zilizopo ili kutoa fursa kwa wakulima na wafugaji kujikita katika uzalishaji na kuachana na migogoro. Ikumbukwe kuwa zaidi ya asilimia 70 ya watanzania wote wanaishi vijijini na wanajihusisha zaidi na kilimo pamoja na ufugaji. Mikakati inayoibuliwa na serikali kuhusu uboreshwaji wa sekta kama za kilimo, madini na utalii, inatakiwa pia kuelekezwa kwenye sekta ya ufugaji hususan ufugaji wa asili ambao unahusishwa na migogoro yote hii.

# Wananchi wanasemaje JUU YA MIGOGORO YA ARDHI?

*Na. Valentin Ngorisa*

## MARTHA LAURENT SUMAYE; HANANG. KATIBA NI DAWA YA MIGOGORO YA ARDHI



Migogoro mingi ya ardhi inasababishwa na matumizi ya ardhi kati ya wafugaji, wakulima na wawekezaji ambao aina ya matumizi hairuhusu kuchanganya na hivyo kuleta migongano lakini mgongano huu unaongezwa na serikali kutokuwa na utashi wa kutatua kwa kutekeleza sheria za ardhi japo angalau kwa sehemu fulani. Kuongezeka kwa watu, mifugo, mahitaji makubwa ya ardhi ya kilimo na kiangazi cha muda mrefu ni vichocheo vikubwa vya migogoro ya ardhi. Ili kuweza kutatua migogoro ya muda mrefu na inayoibuka ya ardhi ni lazima suala la Ardhi liwe la Kikatiba ili kuweza kulinda ipasavyo.



## SAIDI KINDAMBA: MWANGALIZI WILAYA MOROGORO: SHERIA IWEPO YA KUWABANA WATENDAJI WA WILAYA

Migogoro mingi ya ardhi huasababishwa na kutokuwepo kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika nchi nzima unaotokana na matakwa ya wananchi na pale ambapo mpango upo watendaji wa serikali hasa kuanzia ngazi ya Kijiji na Wilaya hasa Idara ya Ardhi hujihusisha moja kwa moja katika kupora ardhi za wananchi baada ya kupokea hongo kutoka kwa wale wanaotafuta ardhi. Ili kukabiliana na ongezeko kubwa la migogoro ya ardhi ni lazima serikali itunge sheria ya kuwabana maofisa hasa Idara ya ardhi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na iweke wazi kuwa pale ambapo wataambatana na wawekezaji ni lazima wananchi wajulishwe faida na hasara za uwekezaji katika ardhi hasa pale ambapo Ardhi ikishatolewa basi inahama kutoka Ardhi ya Kijiji kwenda Ardhi ya Jumla hivyo kuondoa mamlaka kutoka kwa wananchi.

Pili, mpango wa matumizi bora ya ardhi itolewe nchi nzima na yatakayojumuishwa katika mipango hiyo iwe ni maoni ya wananchi na sio mahitaji ya wawekezaji tu. Tatu, HAKIARDHI na wadau wengine wasichoke kutoa Elimu juu ya masuala ya ardhi na kuwasaidia wale wote wenye uhitaji wa masuala ya ardhi.

## MERCELINA CHARLES: MOROGORO; WAFUGAJI NA WAKULIMA KUWA KITU KIMOJA



Migogoro ya Ardhi yanayotokea baina ya wafugaji na wakulima ni kwasababu wao wenyewe hawajui sababu hasa ya nini kinachowagombanisha wakati walipaswa kuungana na kupambana na adui yao mkubwa ambaye ni wale wanaopora ardhi na kuacha bila kutumia huku wafugaji na wakulima wakibaki kugombea kile kidogo kilichobaki. Ili kuondoa migogoro hii ya ardhi ni vyema kwanza kupatanisha makundi haya makuu yanayozozana na kuwaelemisha juu ya haki zao za ardhi ili wao kwa pamoja waweze kupambana na wale walio na wanaoendelea kupora ardhi zao bila hata kuziendeleza. Pili, Taasisi ya HAKIARDHI na Serikali zishirikiane katika kuchambua na kubainisha aina ya uwekezaji katika nchi na namna bora ya kuwasaidia wananchi wasiendelee kupoteza ardhi zao.

*kundi la ng'ombe likiwa chini ya ulinzi*



# OPERESHENI ONDOA WAFUGAJI NI SULUHU YA MIGOGORO YA WAFUGAJI?


*Kwa zaidi ya miongo miwili sasa kuanzia miaka ya 1990, kumekuwepo na migogoro ya wafugaji na wakulima Tanzania huku sababu kubwa inayoelezwa ikiwa ni wafugaji kuvamia maeneo ya wakulima au kulishia mifugo katika mashamba.*

*Na; Valentin Ngorisa*

Kwa upande mwingine kumekuwepo migogoro baina ya wafugaji na taasisi za kiserikali ikiwemo mamlaka za Hifadhi za wanyamapori kama vile TANAPA na mamlaka za Uhifadhi wa Mazingira hasa maeneo oevu kama vile Ramsar Sites na wakati mwingine baina ya wafugaji na wawekezaji hasa katika sekta ya Utalii wa uwindaji wa wanyamapori. Katika nyakati zote, wafugaji wamekuwa wakilaumiwa na taasisi za kiserikali kuwa ni wavamizi wa hifadhi za taifa na maeneo yaliyotengwa kwa matumizi maalumu.

Takwimu zinaonyesha ongezeko kubwa la maeneo yaliyohifadhiwa nchini. Kwa sasa, Tanzania ina Hifadhi za Taifa 16, Mapori ya Akiba 31, Pori Tengefu 44, Hifadhi za Jamii za Wanyama Pori (WMA) 33, Maeneo Oevu (Ramsar Sites) 4, na Misitu ya Asili (Nature Reserves) 6. Ongezeko hili kubwa la hifadhi za wanyamapori limepunguza kwa kiasi kikubwa maeneo ya malisho ya mifugo. Matokeo yake, wafugaji wamekuwa na mtawanyiko wa takribani nchi nzima na mara nyingine kujikuta katika maeneo yanayotumiwa na makundi mengine hususan wakulima na migogoro kutokea.

Mkakati mkubwa ambao umekuwa ukitumiwa na serikali kuondoa wafugaji



**Kati ya mifugo 56,700 iliyotarajiwa kupelekwa mikoa ya Ruvuma na Lindi, ni 13,000 iliyofika ikiwa hai.**

katika maeneo hayo ni kuendesha operesheni maalumu za kuondoa wafugaji. Opereshni hizi zimekuwa zikitumia nguvu kubwa kupita kiasi na kusababisha uharibifu wa mali na maisha ya wananchi wakiwemo wasio na hatia. Nitajadili baadhi tu ya operesheni zilizoleta maafa makubwa hasa kwa jamii za wafugaji.

Tarehe 30 Desemba 2005, Rais Jakaya Kikwete alitoa hotuba bungeni iliyoweka bayana azma ya serikali ya kuondoa wafugaji katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuhifadhi mazingira. Kauli hii iliweka msingi wa uendeshaji wa operesheni zote zilizofuatia.

Mnamo mwezi Machi 2006 makamu wa Rais alitoa mkakati wa kuokoa maeneo oevu nchini yakiwemo mabonde ya Ruaha na Kilombero ambayo yalikuwa yamevamiwa kwa shughuli za kibinadamu. Mkakati huu ulizaa operesheni ondoa Wafugaji bonde la Ihefu ambao ulianza rasmi tarehe 7 Novemba 2006. Operesheni ondoa wafugaji Ihefu, ilishuhudia wafugaji wakihamishwa kwa nguvu toka Ihefu na kuambiwa wahamie mikoa ya kusini huku wakipoteza zaidi ya mifugo 20,226 kwa kufa njiani, kupotea au kuporwa na waliokuwa wakifanya operesheni.

Licha ya mifugo, mali zilipotea na familia kusambaratika. Hatma ya operesheni hii ilikuwa ni kubadilishwa kwa eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 10,000 zilizokuwa zikitumiwa na wananchi na kufanywa hifadhi ya taifa ya Ruaha. Utafiti uliofanywa na HAKIARDHI 2011 unaonyesha kuwa, kati ya mifugo 56,700 iliyotarajiwa kupelekwa mikoa ya Ruvuma na Lindi, ni 13,000 iliyofika ikiwa hai. Bila shaka kuna mifugo iliyoishia maeneo mengine kama Ulanga na Kilombero ambako migogoro mikubwa imeshuhudiwa mara tu baada ya operesheni ya Ihefu kukamilika.

Mnamo mwaka 2012, ilifanyika operesheni nyingine ondoa wafugaji Ulanga na Kilombero. Kama ilivyokuwa kwa Ihefu, ongezeko la wafugaji wa Kilombero na Ulanga ni matokeo ya kupanuliwa kwa maeneo ya hifadhi za Taifa na operesheni ondoa wafugaji kutoka maeneo mengine. Kilombero na Ulanga yanaelezwa kuwa ni maeneo yaliyo katika urithi wa ardhi oevu kidunia (Ramsar Sites) na pori tengefu la Selou. Katika operesheni hii, zaidi ya watu 5,000 na mifugo 486,000 waliondolewa huku wafugaji 5 wa jamii ya Kisukuma wakipoteza maisha wakiondolewa kinguvu na jeshi la polisi bila ya kuonyeshwa wapi pa kwenda.

Eneo jingine ambalo wafugaji wamekuwa wakiondoshwa kwa operesheni za mara kwa mara ni Loliondo katika Wilaya ya Ngorongoro. Mwaka 1992 serikali ilitoa haki za uwindaji kwa Kampuni ya Ottelo Business Cooperation (OBC), katika eneo ambalo kwa sehemu kubwa linatumiwa na jamii za wafugaji kuendesha maisha yao. Tangu hapo, kumekuwa na migogoro isiyoisha kati ya Serikali na Kampuni hiyo kwa upande mmoja na wananchi wanaozunguka eneo hilo kwa upande mwingine hasa kutokana na serikali kuendesha operesheni za kuwaondoa wafugaji kutoka maeneo ambayo ni malisho wakati wa kiangazi.

Katika operesheni ya mwaka 2009 zaidi ya mifugo 50,000 iliondolewa katika eneo hilo huku mingi ikipotea na kuliwa na wanyamapori na zaidi ya maboma 200 yalichomwa moto. Hivi sasa, zaidi ya watu 40,000 wanatarajiwa kuondolewa endapo mkatati wa serikali wa kumega kilomita za mraba 1,500 kutoka kwenye maeneo ya wananchi ili yawe sehemu ya hifadhi utafanikiwa.

Uendeshaji wa operesheni zote hizo na nyingine nyingi ambazo hazitajwi unaacha maswali mengi kuliko majibu. Kwa mfano, je ufugaji wa asili na wafugaji wana nafasi gani katika kupata, kumiliki na kutumia rasilimali ardhi, malisho na maji kama ilivyo kwa makundi mengine?. Je ni nini kinakwamisha upangaji wa matumizi ya ardhi ili wafugaji wawe na maeneo ya uhakika kwa malisho kama ilivyo kwa makundi mengine na ardhi yao ikaheshimiwa? Je operesheni ni njia muafaka ya kuepusha migogoro kati ya wakulima na wafugaji au ni namna ya kuhamishia tatizo maeneo mengine?. Serikali kuu na serikali za mitaa kwa pamoja wakiweza kujibu na kuyafanyia kazi maswali haya kwa ufasaha, migogoro ya ardhi itakuwa historia na haitasikika tena operesheni yoyote iwe kwa wakulima au wafugaji.



# SHERIA YA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI (SURA YA 2I2) YA MWAKA 2002 IBORESHWE

***Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuweka mfumo wa kuratibu milki, usimamizi na matumizi ya ardhi kwa kutunga sera ya Taifa ya ardhi ya mwaka 1995 na sheria za Ardhi za mwaka 1999.***

*Na; Beatha Fabian*

Aidha, mfumo wa utatuzi wa migogoro umewekewa utaratibu kwa sheria maalum ya mabaraza na mahakama za utatuzi wa migogoro ya ardhi namba 2 ya mwaka 2002. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto nyingi za kiutendaji wa mamlaka zinazohusika na usimamizi na utatuzi wa migogoro kiasi cha kushuhudia migogoro ya ardhi kuendelea kuongezeka badala ya kupungua kutokana na kuwepo kwa sheria hizi.

Changamoto hizi kama zilivyoainishwa na utafiti uliofanywa na Tume ya kurekebisha sheria Tanzania ni pamoja na; Vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi kusimamiwa na mamlaka tofauti.Mathalan mabaraza ya ardhi ya vijiji na Kata yapo chini ya wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mabaraza ya ardhi na Nyumba ya Wilaya yanasimamiwa na wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa zipo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria. Changamoto hii inasababisha ugumu kwenye utendaji na usimamizi wa vyombo hivi hususani mamlaka kamili baina ya hivi vyombo, uwajibikaji, uhuru wa watendaji, na nidhamu kutokana na uwepo wa mamlaka tofauti zinakowajibika. Hali hii imepunguza ufanisi wa vyombo hivi katika utatuzi wa migogoro ya ardhi. Kwa kuwa vyombo hivi vinajihusisha na utoaji haki, kumekuwa na mapendekezo kuwa maboresho ya sheria yajikite katika uundwaji unaosimamiwa na mhimili wa mahakama iliyopewa dhamana ya haki kikatiba.

Maboresho mengine ya msingi yafanywe katika kifungu cha 2 na 10 ili kuruhusu mabaraza ya kata na wilaya yaliyoko mijini yawe na nguvu ya kusikiliza migogoro ya ardhi kwani kumekuwepo na hukumu zinazoyanyima mamlaka ya kusikiliza kesi za ardhi.

Tafsiri ya ardhi katika sheria hii ya utatuzi wa migogoro ya ardhi imeminywa na hivyo maboresho katika kifungu cha 2 cha sheria hii yafanyike ili kuruhusu maana ya ardhi kutafsiriwa kwa mujibu wa sheria za ardhi za mwaka 1999

Pia, sheria iruhusu uwakilishi wa wakili katika mabaraza ya kata kwani katika maeneo ambako HAKIARDHI imefanya kazi inaonesha kuwa watu wanaoshitakiwa au kufungua kesi za ardhi katika Mabaraza ya Kata hawana uelewa wa kutosha na wamekuwa wakiomba fursa hiyo ambayo ni haki ya Kikatiba na kukataliwa (rejea kesi ya Fans William Muze V. Kalumela Mula Misc Land Appeal Case 3,2008). Maboresho katika Kifungu hiki cha 18 yatasaidia watu wasioweza kuwakilisha madai yao na pia kupata haki zao na usaidizi zaidi pale wanapoitaji kukata rufaa


Katika upande wa wasaidizi wa mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, ni vyema kuongeza sifa za wasaidizi hao ya taaluma ya uanasheria maana sheria ipo kimya katika kifungu cha 27. Hii itasaidia kuboresha mchango wao

katika kesi au ushauri wa kisheria ambao unatolewa nao katika ngazi hii kwani kesi katika mabaraza haya zinahusisha kwa kiasi kikubwa sheria, taratibu na kanuni mbalimbali.

Moja ya misingi ya haki asilia ni pamoja na kujua hukumu inayotolewa pamoja na sababu za kufikia hukumu husika. Katika Ngazi ya Baraza la Ardi na Nyumba la wilaya kumbukumbu za kesi pamoja na hukumu huandaliwa kwa lugha ya Kiingereza tu. Sheria ifanyiwe marekebisho katika kifungu cha 32 kuruhusu lugha ya Kiswahili kutumika. Hii ni pamoja na mahakamu zingine za juu pia.

Kutokana na gharama za ardhi kupanda na kubadilika mara kwa mara, uzoefu wa kesi nyingi zinazofunguliwa ngazi ya baraza la Kata ni zaidi ya milioni 3. Sheria ibadilishe ukomo wa kifedha uwe ni kwa ardhi yenye thamani isiyozidi milioni 10 badala ya milioni 3. Pia katika kifungu cha 33 (2) ukomo wa kifedha kwa Mabaraza ya ardhi na Nyumba ya wilaya uwe ni kwa ardhi yenye thamani isiyozidi milioni 100 badala ya milioni 50 na pia kwa mali inayohamishika thamani yake isizidi milioni themanini badala ya milioni arobaini

Haya ni baadhi ya maboresho ya muhimu ambayo Bunge likiyafanya yatasaidia malengo na makusudio ya Sheria hiyo kutekelezwa kwa ubora na mafanikio zaidi. Pia, serikali kupitia vyombo hivi itawezesha utatuzi na usuluhishi wa migogoro ya ardhi kufanyika kwa urahisi, kudumisha ushirikiano na amani kati ya wakulima na wafugaji na serikali kwa ujumla. Uamuzi ukifanyika kwa wakati utaondoa tatizo la urasimu uliopo, vikwazo na mlundikano wa kesi na pia utapunguza gharama za kiutawala katika kuendesha mashauri ya ardhi.







# ARDHI NI UHAI

HAKIARDHI ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 13 JANUARI - APRILI 2015



*Washiriki wa kongamano la maadhimisho ya miaka 20 ya HAKIARDHI wakiwa katika picha ya pamoja kwenye ukumbi wa LandMark Hotel Dar es Salaam.*

## BAADHI YA MACHAPISHO

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ardhi ni Uhai 1995 | Georgis Hadjiyavanis |
| 2. | Not yet Democracy: Reforming Land tenure in Tanzania 1998 | Issa G. Shivji |
| 3. | Haki za Wamasai waishio Ngorongoro 1999 | Issa.G Shivji/Wilbert Kapinga |
| 4. | Mwongozo wa haki za Ardhi kwa wananchi wa Tanzania 2002 | Issa G.Shivji/Deus Kibamba |
| 5. | Silencies in NGOs Discourse Occasional paper No.1 2006 | Issa G.Shivji |
| 6. | The mute Plunder "Bioreosurces and disposesion in Tanzania 2008 | Ng'wanza Kamata |
| 7. | Public Perceptions on bioresources conservation in Tanzania 2008 | HAKIARDHI |
| 8. | Accumulation by land dispossession and labor devaluation 2011 | HAKIARDHI |
| 9. | Biofuels in Tanzania 2013 | HAKIARDHI |
| 10. | Local people's perception on climate change in Tanzania 2013 | Cathbert Tomitho |
| 11. | Land grabbing in a post investment Rufiji basin 2013 | Mwami&Kamata |
| 12. | Ardhi iwe nguzo katika katiba mpya 2014 | HAKIARDHI |